Atakapotoa matumizi mtu kwa familia yake kwa kutaraji malipo, basi hiyo kwake ni sadaka

Imepokelewa kutoka kwa Abuu Masoud -Radhi za Allah ziwe juu yake- kutoka kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- amesema: "Atakapotoa matumizi mtu kwa familia yake kwa kutaraji malipo, basi hiyo kwake ni sadaka".

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Anaeleza Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- yakuwa atakapotoa mtu matumizi kwa familia yake, wale anaolazimika kuwahudumia kama mke wake na watoto wake na wengineo huku akijikurubisha kwa Allah Mtukufu kwa hilo, na akitaraji malipo kwake kwa yale anayowahudumia basi atakuwa na malipo ya sadaka.

http://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/6460